**MAKABIDHIANO YA NDEGE AINA YA FOKKER 50 KATI YA SERIKALI (TGFA) NA SHIRIKA LA NDEGE LA TANZANIA (ATCL)**

**MAELEZO MAFUPI (TALKING NOTES) YA KATIBU MKUU KIONGOZI**

---

***Dkt. Leonard Chamuriho, Katibu (Uchukuzi),***

***Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu Ikulu,***

***Mhandisi Ladislaus Matindi, Mtendaji Mkuu wa ATCL,***

***Bwana Benjamin Ndimila, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ndege za Serikali,***

***Maafisa wote mliopo,***

***Mabibi na Mabwana.***

Habari za mchana.

Awali ya yote, nachukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kutukutanisha sote mahali hapa kwa shughuli hii ya kukabidhi ndege ya Serikali kwa ATCL.

Wote tunakumbuka maagizo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyotoa tarehe 11 Januari 2019, wakati wa hafla ya mapokezi na makabidhiano ya ndege aina ya Airbus 220-300 iliyofanyika hapa hapa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (Julius Nyerere International

Airport (JNIA). Pamoja na masuala mengine, Mheshimiwa Rais, aliagiza kwamba ndege mbili za Serikali, aina ya **Fokker 50 na Fokker 28** ambazo zinatumika kwa safari za Viongozi Wakuu wa Serikali nazo ziwekwe nembo (zipakwe rangi na kuchora picha ya Twiga) ya Air Tanzania na zikodishwe kwa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) ili ziweze kutumika kubeba abiria kwa sababu si kila wakati zinatumika kwa ajili ya shughuli za Serikali.

Maagizo haya ni miongoni mwa juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano kuhakikisha kwamba usafiri wa anga nchini unaimarika na wananchi wanawezeshwa kufanya shughuli zao za maendeleo na za kijamii kwa urahisi na kwa haraka zaidi. Sote tunafahamu kwamba hadi sasa Serikali imeshanunua ndege mpya sita (6) ambazo ni: **Bombardier Q400-8** (3), **Boeing 787-8 Dreamliner** (1), na **Airbus 220-300 (2)**. Ndege zote sita zimekodishwa kwa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na zinafanya kazi. Ndege nyingine mpya mbili zaidi, ambazo ni **Boeing 787-8 Dreamliner** na **Bombardier Q400-8**), zimeagizwa na zinatarajiwa kuwasili nchini mwishoni mwa mwaka huu.

Pamoja na kwamba utaratibu huu wa Serikali wa kukodisha ndege zake kwa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) unalenga kuliimarisha Shirika hili ili liweze kuhimili ushindani katika sekta ya usafiri wa anga, Serikali pia inalenga kupata mapato kupitia tozo ya kukodisha ndege hizo kwa ATCL. Ninafahamu kwamba ATCL wamekuwa wakilipa tozo hii kila mwezi, ingawa wakati mwingine malipo yamekuwa yakichelewa. Ningependa kuwakumbusha ATCL

kwamba mnapaswa kufanya malipo haya **kwa wakati na kwa kiwango kilichokubaliwa**. Ikumbukwe kuwa fedha hizi zinahitajika ili kununua ndege nyingine, au kupangiwa matumizi mengine kwa ajili ya kuwaletea wananchi maendeleo.

Aidha, mbali na Shirika la Ndege la Tanzania kuilipa Serikali tozo ya kukodisha ndege, **Shirika hili kama mashirika mengine ya umma pia linapaswa kutoa gawio kwa Serikali kutokana na faida inayotokana na biashara yake**. Hivyo, ningependa kutumia fursa hii kuikumbusha Menejimenti ya ATCL kufanya kazi kwa weledi kwa lengo la kupata ufanisi, ili kuliwezesha Shirika kupata faida na hivyo kuweza kutoa gawio kwa Serikali kila mwaka. Ni lazima matunda ya uwekezaji unaofanywa na Serikali katika sekta ya usafiri wa anga yaonekane.

Tumekutana leo kuteleleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya kulikadidhi Shirika la Ndge la Tanzania ndege moja aina ya Fokker 50 yenye usajili 5H-TGF. Hatua hii ni baada ndege hii kuwekwa nembo na rangi ya Air Tanzania. Ndege hii sasa iko tayari kuanza kutumika kwa ajili ya kubeba abiria.

Ndege hii ina uwezo wa kutua viwanja vyote nchini ikiwemo viwanja vya ndege vyenye lami na visivyokuwa na lami, ikiwa pamoja na viwanja vifupi ambavyo ndege kubwa haziwezi kutua. Ndege hii iko katika hali nzuri na imekuwa ikitoa huduma kwa Viongozi Wakuu wa Serikali. Ndege hii pia imekua ikihudumiwa na wataalamu wazalendo

wenye mafunzo kamili na wenye uzoefu wa kutosha. Ni matumaini ya Mheshimiwa Rais, pamoja na watanzania wote kwamba, kwa kupata ndege hii, huduma za usafiri wa anga zitaimarika zaidi, na itawaongezea ATCL uwezo kwa kuongeza wigo wa mtandao wa kutoa huduma (*routes)* ili kuweza kuwafikia wananchi wengi zaidi. Ninafahamu kwamba ndege nyingine, aina ya Fokker 28 iko katika matengenezo na mara baada ya kukamilika, nayo pia itakabidhiwa kwa ATCL kwa ajili ya kuanza kutumika kubeba abiria.

**Mwisho,** ningependa kuwakumbusha na kuwasisitiza kuzingatia maelekezo ya Mheshimiwa Rais juu ya umakini katika matumizi ya fedha na raslimali za umma. Daima kumbukeni kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inalenga kuwakwamua Watanzania kutoka kwenye umaskini. Kila uwekezaji unaofanywa na Serikali unalenga kuongeza mapato kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa ajili ya faida ya wananchi wote, hususan wanyonge. Hivyo, haitarajiwi kuona mali za umma zikitumika kwa malengo tofauti na malengo na maagizo ya Serikali. Aidha, ni matarajio ya Mheshimiwa Rais kwamba mtakuwa wabunifu zaidi ili kuepuka matumizi makubwa ya fedha kwa shughuli ambazo zinaweza kufanywa kwa gharama nafuu kama ubunifu na uzalendo vitazingatiwa katika utendaji kazi wenu.

**Baada ya maelezo haya mafupi, sasa niko tayari kukabidhi ndege hii aina ya Fokker 50 yenye usajili 5H-TGF kwa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) kwa ajili ya matumizi ya biashara kwa masharti na taratibu zilizowekwa kwenye mkataba wa makabidhiano.**